Kielelezo cha taarifa kuhusu Watoto Wachanga Tanzania

Mtoto mchanga akizaliwa hai, lakini akafa kabla ya kutimiza mwezi mmoja (wakati mwingine ina maana ya ndani ya 28) huitwa kifo cha mtoto mchanga[1]. Zaidi ya asilimia 80 ya vifo vyote vya watoto wachanga vinatokana na sababu tatu zinazozuilika na kutibika:

- Matatizo yanayotokana na kuzaliwa kabla ya muda (njiti)
- Maambukizi kwa watoto wachanga kama yale yatokanayo na bakteria
- Matatizo wakati wa kujifungua ikiwemo kushindwa kupumua[1]

Maisha ya watoto hawa yanaweza kuokolewa kama huduma bora wakati wa kujifungua zitapatikana, uwepo wa dawa na kuchukua hatua nyingine rahisi .

Vifo vya watoto wachanga ni janga la afya ya jamii Tanzania

Kila mwaka takribani watoto wachanga 39,000 hufariki kabla ya kutimiza mwezi mmoja hapa Tanzania, na hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi ya 11 duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya vifo vya watoto wachanga ulimwenguni[2]. Kipindi cha kujifungua ni kipindi muhimu sana. Zaidi ya theluthi moja ya vifo hutokea wakati wa kuzaliwa, na asilimia 73 ndani ya wiki moja[3]. Kwa mwaka mmoja watoto wachanga wa Tanzania 13,900 hufariki katika siku yao ya kwanza ya kuzaliwa, na watoto wachanga 28,200 ndani ya wiki moja tangu kuzaliwa[3].

Kati ya takribani watoto wachanga 39,000 wanaofariki Tanzania, 11,900 (31%) hufariki kutokana na matatizo wakati wa kujifungua, 9,400 (24%) wanakufa kutokana na matatizo ya kuzaliwa njiti, na watoto 7,800 (20%) hufariki kutokana na maambukizi kama yale ya bakteria au uti wa mgongo[4]. Vile vile watoto wengine 22,000 huzaliwa wafu wakifariki wakati wa kuzaliwa. Vifo hivi vinaashiria uhitaji wa haraka wa kuwepo wahudumu wa afya wenye ujuzi na huduma bora wakati wa kujifungua mahali pote nchini Tanzania.

Ingawa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kushughulikia vifo vya watoto kwa ujumla wake na tayari imefikia lengo la nne la milenia la kupunguza vifo vya watoto, maendeleo katika swala la uhai wa watoto wachanga yamekua ya kasi ndogo kiasi kwamba hivi sasa vifo vya watoto wachanga vinachangia asilimia 40% ya vifo vyote vya watoto.[2]

Nini kinaweza kufanyika Tanzania?

Kutokomeza vifo vya watoto wachanga vinavyozuilika kunahitaji kuwekeza katika kuboresha huduma za afya na zile za mama na mtoto mchanga, na vile vile kuhakikisha wahudumu wenye ujuzi na wenye nyenzo zote muhimu kiutendaji wakati wanamhudumia kila mama kujifungua ikiwemo:

- Kuwekeza katika huduma bora wakati wa kujifungua, na baada ya kujifungua
- Huduma maalum kwa watoto wenye uzito mdogo na wanaoumwa
- Kupunguza pengo la uwiano: Kila uzazi unapaswa kuhudumiwa na mtoa huduma mwenye ujuzi na vifaa
- Kuhamasisha kupangilia uzazi kwa muda wa kutosha ili kupunguza uzazi wa watoto njiti kwa kupitia kunyonyesha kwa miezi 24 na matumizi ya uzazi wa mpango pamoja na huduma bora za akina mama kabla, wakati na baada ya ujauzito, na hasa miongoni mwa vijana wa umri chini ya miaka ishirini
- Kuhamasisha unyonyeshaji wa maziwa ya mama mapema na kunyonyesha maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya mwanzo
- Kuboresha afya na usafi wa mazingira, ikiwemo vyoo katika vituo vya huduma za afya, sambamba na kuhakikisha uwepo wa dawa muhimu ikiwemo antibiotiki, ili kupunguza vifo vya watoto wachanga vitokanavyo na maambukizi ya bakteria na aina zingine [1,5]

Mwaka 2014 Tanzania iliweka dhamira ya kutekeleza Mpango Kazi wa Kila Mtoto Mchanga[1] na Mpango Mkakati Ulioboreshwa[5]. Mikakati hii inaonyesha wazi vipaumbele ambavyo ni suluhu kwa matatizo haya, inahimiza nguvu za pamoja ili kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo vya akinamama na watoto wachanga, na kuepusha tatizo la watoto wanaozaliwa wafu. Ni wajibu wetu kuweka vipaumbele kulingana na ushahidi, vyenye gharama nafuu na vya kutekelezeka katika vituo vyote vya afya vinavyohudumia wajawazito na kutoa huduma za kujifungua. Vile vile kuhakikisha ukusanyaji bora wa takwimu juu ya matokeo ya ujauzito ili kuwezesha hatua stahiki kuchukuliwa pale zinapohitajika zaidi.

Kama mpango mkakati ulioboreshwa utatekelezwa, maisha ya watoto wachanga 9,400 yaweza kuokolewa na kuepusha watoto 2,500 kuzaliwa wafu na kuzuia vifo vya akina mama vipatavyo 1,400 ifikapo Desemba 2015

Watoto wachanga Tanzania

Idadi ya watoto wachanga wanaofariki ndani ya mwezi mmoja wa uhai wao (2013)	**38,600**
Idadi ya watoto wachanga wanaofariki katika siku ya kwanza ya kuzaliwa (2013	13.900
Kiwango cha vifo ndani ya mwezi mmoja tangu kuzaliwa	**21 kwa kila vizazi hai 1,000**
Nafasi ya nchi kimataifa, kuhusiana na idadi ya vifo vya watoto wachanga (2013)[2]	11th
Idadi ya watoto wanaozaliwa kabla ya muda (2013)[6]	**213,500**
Idadi ya vifo vitokanavyo na matatizo ya kuzaliwa kabla ya muda (njiti)	9,400
Idadi ya vifo vinavyotokea wakati mama anajifungua (2013)[4]	**11,900**
Idadi ya vifo vitokanavyo na maambukizi ya bakteria/homa ya uti wa mgongo/ pepopunda (2013)[4]	7,800
Mahitaji ya huduma ya uzazi wa mpango yaliyokidhiwa (2010)[8]	**58%**
Mahudhurio ya kliniki ya wajawazito mara nne au zaidi (2010)[8]	43%
Kiwango cha akinamama wanoaosaidiwa na wahudumu wenye ujuzi wakati wa kujifungua (2010)[8]	**49%**
Kiwango cha akinamama na watoto wachanga wanaopata huduma baada ya kujifungua ndani ya siku mbili za awali(2010)[8]	31%
Kiwango cha kunyonyesha watoto wachanga maziwa ya mama mapema (ndani ya saa moja ya kuzaliwa)(2010)[8]	**49%**
Kiwango cha kunyonyesha maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya mwanzo (2010)[8]	50%

Marejeo

1. World Health Organization, & UNICEF. (2014). Every Newborn: An Action Plan to End Preventable Deaths. Geneva: WHO.
2. UNICEF. (2014). *Committing to Child Survival: Progress Report 2014 Committing to Child Survival: A Promise Renewed*. New York: United Nations Children's Fund.
3. Oza S., Cousens S., Lawn JE. (2014). Estimation of daily risk of neonatal death, including the day of birth in 186 countries in 2013: a vital-registration and modelling-based study. *Lancet Global Health, 2*(11): e635-e644
4. Liu, L., Oza, S., Hogan, D., Perin, J., Rudan, I., Lawn, J. E., Cousens, S., Mathers, C., & Black, R. E. (2014). Global, regional, and national causes of child mortality in 2000—13, with projections to inform post-2015 priorities: an updated systematic analysis. Supplementary appendix. *The Lancet*, *(Early online publication)*.
5. Ministry of Health and Social Welfare [United Republic of Tanzania]. (2014). *The National Road Map Strategic Plan to Accelerate Reduction of Maternal Newborn and Child Deaths in Tanzania 2008-2015. Sharpened One Plan April 2014*. Dar Es Salaam: MoHSW
6. Blencowe, H., Cousens, S., Oestergaard, M. Z., Chou, D., Moller, A.-B., Narwal, R., Adler, A., Garcia, C.V., Rhode, S., Say,L., & Lawn, J. E. (2012). National, regional, and worldwide estimates of preterm birth rates in 2010 with time trends since 1990 for selected countries: a systematic analysis and implications. *The Lancet*, *379*(9832), 2162–2172
7. United Nations Population Division. (forthcoming, 2014). World Population Prospects: The 2013 Revision [estimates for 2013 used].
8. National Bureau of Statistics [Tanzania], & ICF Macro. (2010). *Tanzania Demographic and Health Survey 2010*. Dar Es Salaam/Calverton: NBS, ICF Macro.
9. World Health Organization. (2005). *Report of a WHO Technical Consultation on Birth Spacing Geneva, Switzerland 13–15 June 2005.* Geneva: WHO.
10. Evidence for Action. (2014). *MamaYe Facts and Figures on Breastfeeding*. London: Evidence for Action.

Maelezo:

a. Muda wa miezi sita au pungufu kati ya kujifungua na mimba unaongeza uwezekano wa vifo vinavyotokana na matatizo ya ujauzito. Kipindi cha miezi 18 au pungufu kinaongeza uwezekano wa vifo vya watoto wachanga (umri hadi siku 28), watoto chini ya mwaka mmoja, watoto kuanzia wiki 22 baada ya mimba kutungwa hadi siku saba baada ya kuzaliwa, mtoto kuzaliwa na uzito pungufu, watoto wadogo kulinganisha na umri wa mimba na kuzaliwa kabla ya wakati. Shirika la Afya Duniani (WHO) linashauri kipindi cha miezi 24 kati ya ujauzito mmoja hadi mwingine[9]

b. Nchini Tanzania, inakadiriwa kuwa kulikuwa na vizazi hai 1,865,300 mwaka 2013 na kiwango cha uzazi wa watoto kabla ya muda wa 11.4%[6] mwaka 2010. Kama kiwango cha uzazi wa watoto kabla ya muda na idadi ya vizazi hai vya mwaka 2013 vitatumiwa kukokotoa idadi ya watoto waliozaliwa kabla ya wakati (njiti) watoto njiti wapatao 11.4/100*1,865,300=213,490 walizaliwa mwaka 2013 (inayokadiriwa kama 213,500). Kiwango cha uzazi wa watoto kabla ya wakati cha 11.4% ni sawa na mtoto mmoja kwa kila watoto tisa wanaozaliwa hai. Nchi zimepangwa kufuatana na makadirio ya mwaka 2013

c. Kiwango cha vifo kutokana na matatizo yanayotokana na kuzaliwa kabla ya wakati katika siku 28 za mwanzo nchini Tanzania (iliyokadiriwa toka 9, 394)[4] . Kama vifo vitokanavyo na matatizo ya kuzaliwa njiti vitahusishwa toka kuzaliwa hadi miaka mitano, namba hii inakuwa 10,800 (Makadirio yaliyotolewa na Save the Children).

November 2014